

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**



TAMKO

**YAH: VIDEO FUPI INAYOSAMBAA MITANDAONI IKIONYESHA WATAALAMU WA
AFYA WAKIBISHANA JUU YA VITENDANISHI VYA MAABARA**

2. Baraza la wataalam wa Maabara (Health Laboratory Practitioners Council-HLPC) linakiri kuona video fupi inayozunguka kupitia mitandao ya kijamii, ukiwemo mtandao wa "WhatsApp" inayohusisha mtumishi wa Afya aliyevalia sare za kazi (sare za uuguzi) na mtumishi mwingine asiyevaa sare za kazi (aliyebainika kuwa ni Mtalaam wa Maabara)
3. Aidha, Baraza linalaani kitendo cha Watumishi hawa wa umma kutumia lugha zisizo na staha, kisha kujirekodi na kutuma video hiyo kwenye mitandao ya kijamii kinyume na maadili ya utumishi wa umma. Kama hiyo haitoshi, Baraza linalaani vikali kwa muuguzi wa kituo hicho (jina limehifadhiwa) kumtaka Mtalaam wa Maabara kutekeleza kitendo cha kufanya kipimo cha Malaria "Malaria Rapid Diagnostic test" kwa kutumia vitendanishi vinavyohisiwa kuisha muda wake wa Matumizi. Vitendo hivi ni kinyume na sheria, kanuni na maadili ya taaluma na utumishi wa umma.
4. Kufuatia kitendo hicho ambacho hakikubaliki, Wizara ya Afya kupitia Baraza la Wataalam wa Maabara limechukua hatua za haraka kufanya ufuatiliaji na Uchunguzi wa haraka katika kituo hicho ili kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watumishi hao na wengine watakaobainika kushiriki katika kitendo hicho. Aidha, timu ya wataalam kutoka Ngazi ya Mkoa na Halmashauri imeshafika kituoni kwa ajili ya Uchunguzi huu.
5. Aidha, Baraza la Wataalamu wa Maabara linatoa rai kwa Wataalam wote wa Maabara nchini, kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kusimamia Miiko na Maadili ya taaluma yao na kwa kufuata miongozo ya kutoa majibu ya vipimo vya Maabara. Vile vile, Baraza linawakumbusha Wataalamu kufuata taratibu za utumishi wa umma za kuripoti changamoto za kinidhamu katika sehemu zao za kazi.

Limetolewa na



Zubeda M. Salum

Naibu Msajili, Baraza la Wataalam wa Maabara

06 Januari, 2023